

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**



**SIMU NA:** +255 252957128

S.L.P 216,  
**MPANDA – KATAVI.**

**FAX NA:** +255 252957129

**TANGAZO**  
**ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA USAFI KATIKA KITUO CHA MABASI ILEMBO KWA**  
**KIPINDI CHA OCTOBA 2018 HADI JUNI 2019**

**ZABUNI No:LGA.101/2018/2019/CQ/NC/05**


Tarehe: 18/09/2018

Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda inakaribisha maombi ya Zabuni kutoka kwenye Taasisi /Mashirika/Makampuni na watu binafsi wenye uwezo, leseni, uzoefu na sifa za kutoa huduma ya Usafi kwenye kituo cha Mabasi Ilembo kwa kipindi cha kuanzia Octoba 01, 2018 hadi Juni 30, 2019.

Zabuni ya kutoa Huduma ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwari hapo chini:-

| S/N | NAMBA YA ZABUNI            | MAELEZO YA ZABUNI  |
|-----|----------------------------|--|
| 1.  | LGA.101/2018/2019/CQ/NC/05 | <p>Zabuni ya Huduma ya usafi katika kituo cha Mabasi Ilembo katika maeneo yafuatayo:-</p> <ul style="list-style-type: none"><li>• Kufanya usafi eneo lote la kituo cha mabasi la nje na ndani.</li><li>• Kufanya usafi wa vyoo vyote na bafu ndani ya kituo cha mabasi kwa kutumia dawa.</li><li>• Kusafisha na kuzibua mitaro ya maji ya mvua na maji taka.</li><li>• Kuweka vifaa kwa ajili ya kukusanyia taka ngumu<br/>Skip bucket 1<br/>20 Dust bin za kilo 100</li><li>• Kukusanya taka ngumu na kuzipeleka eneo lililoandaliwa kwa muda</li><li>• Kutunza nyasi, maua na kupanda mengine inapobidi</li><li>• Kufyeka na kuondoa nyasi nje na ndani ya uzio wa kituo cha mabasi.</li></ul> |

2. Maombi yote ya Nukuu za Bei yazingatie masharti yafuatayo:-
- i) Nyaraka za Nukuu za bei zitapatikana mara baada ya Mwombaji kutembelea eneo la kazi kabla ya kuchukua nyaraka ya zabuni ambayo itatolewa baada ya kutembelea eneo la kazi.
  - ii) Ombi la Nukuu za bei liwe na jina na anuani halisi ya mwombaji, aidha aonyeshe mahali ofisi zake zilipo au anapoweza kupatikana (physical address)
  - iii) Mwombaji awe na ofisi inayojulikana mahali ilipo na itambulike kisheria.
  - iv) Zingatia kuwa fomu ya maombi ya Nukuu za bei inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (power of Attorney) katika zabuni hii.
3. Nukuu zote za bei ziwe na nakala halisi (Original) na nakala mbili zinazofanana (Copy) zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa, "Nukuu ya Bei Na.LGA.101/2018/2019/CQ/NC/05" Huduma ya Usafi katika kituo cha Mabasi Ilembo. Ni lazima kupelekwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabun ya Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, S.L.P 216, MPANDA.
4. Mwisho wa kupokea Nukuu za bei ni saa nne (4) kamili asubuhi (saa za Afrika Mashariki) ya tarehe 24 Mwezi Septemba, 2018 katika ofisi za Halmashauri ya Manispaa, Kitengo cha Ununuzi (PMU) S.L.P 216, Mpanda. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo katika ukumbi wa Halmashauri
5. Tangazo hili ni la **siku 7** tangu tarehe **18/09/2018 hadi 24/09/2018** majira ya Saa **Nne kamili asubuhi**.
6. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa, Sehemu ya Zabuni, Zabuni za kielekitroniki (e-mail), Zabuni ambazo hazitapokelewa, Zabuni ambazo hazitafunguliwa na kusomwa hadharani katika tukio la Ufunguzi wa Zabuni hazitakubalika kufanyiwa tathmini katika hali yoyote ile.



Michael F. Nzyungu  
Mkurugenzi wa Manispa  
**MPANDA-KATAVI**